## 1.0.UTANGULIZI

### 1.1.Mapitio ya Halmashauri

Wilaya ya Ileje ilianzishwa rasmi mwaka 1975 na Halmashauri ya Wilaya ya Ileje ilianzishwa rasmi tarehe 1 Januari 1984 chini ya Kifungu Na. 7 cha Sheria za Serikali za Mitaa ya mwaka 1982. Kuanzia mwaka 1961 – 1974 Wilaya ya Ileje ilikuwa ni sehemu ya Kata na Tarafa ya Rungwe na Mbozi. Jina la Ileje lilitokana na Milima wa Ileje uliokuwepo kabla ya Uhuru.

### 1.2 Idadi ya watu

Kutokana na takwimu za sensa ya 2012 idadi ya watu ilikuwa 124,451 wakiwemo wanawake 65,988 na wanaume 58,463. Kwa makadrio ya watu ya kwa mwaka 2016 idadi ya watu ni 140,055 kati yao wanaume ni 65,793 na wanawake ni 74,262 sawa na ongezeko la asilimia 12.5% katika kipindi cha miaka minne (4).

### 1.3. Mfumo Utawala

Ileje imegawanywa katika tarafa mbili ambazo ni;- Bulambya na Bundali ambazo zimegawanyika katika Kata 18, Vijiji 71 na vitongoji 317 ( Hamlets)


### 1.4 Makabila

Makabila makuu katika wilaya ni Wandali na Walambya ambao wanaishi Bundali na Bulambya. Makabila mengine ni pamoja na Wamalila, Wanyiha, Wanyamwanga na Wanyakyusa.

### 1.5 Mahali ilipo

Wilaya ya Ileje iko upande wa Kusini Magharibi ya Mkoa wa Songwe, na ina eneo la $Km^2$1908. Wilaya inapakana na Wilaya ya Rungwe upande wa Mashariki. Upande wa mashariki Kusini inapakana na Wilaya ya Kyela, Upande wa Kaskazini inapakana na Wilaya ya Mbeya na Upande wa Kaskazini magharibi inapakana na wilaya ya Mbozi na Momba. Upande wa Kusini Wilaya inapakana na nchi ya Malawi ambapo mpaka ni mto Songwe, wakati Kusini Magharibi kuna nchi ya Zambia.

RAMANI YA WILAYA YA ILEJE IKIONYESHA MAENEO YA UTAWALA




## 1.6 Hali ya kijiografia

Ileje inaweza kugawanywa katika kanda tatu (3) –

### (i) Ukanda wa chini

Unapatikana kati ya mita 1300 na 1500, juu ya usawa wa bahari. Sehemu kubwa ipo Tarafa ya Bulambya. Hali ya joto ni kati ya $26^0$ C - $32^0$ C na unapata mvua kati ya mm 750- 100 kwa mwaka. Udongo ni kichanga na wenye rutuba kidogo inayo faa kuzalisha mazao ya msimu kamavile mahindi, ulezi, alizeti, karanga, mpunga, Viazi vitamu na maharage.

### (ii) Ukanda wa juu kaskazini mashariki

Unapatikana kati ya mita **1500 - 1600**, juu ya usawa wa bahari. Sehemu kubwa ipo katika zote mbili za Bulambya na Bundali. Hali ya joto ni kati ya $16^0$ C - $20^0$ C. Inapata mvua kati ya mm 900-1200. Udongo ni mfinyanzi wenye rutuba unaofaa kuzalisha mazao ya kahawa, pareto, mahindi, viazi vitamu na viazi mviringo.

### (iii) Ukanda wa juu mashariki

Ukanda huu ni wamilima ambao upo kati ya mita 1600 and 250 juu ya usawa wa bahali. Wastani wa mvua ni kati ya mm 1500 to 2000. Kiasi cha joto ni kati ya $18^0$ C - $22^0$ C. Udongo ni wavolkano unaofaa kwa kustawisha mazao ya chakula na biashara kama vile migomba, kahawa, mahindi, viazi, maharage na karanga.

## 2.0. HALI YA KIUCHUMI

Uchumi wa Wilaya ya Ileje hutegemea zaidi kilimo na ufugaji ambacho hutoa mchango wa zaidi ya 85% ya pato la Wilaya na 90% ya ajira kwa wakazi wa Wilaya. Kilimo na ufugaji huendeshwa na wakulima wadogo wadogo ambao kwa kiasi kikubwa huendesha kilimo na ufugaji kwa njia za asili/duni. Mazao yanayolimwa ni Mahindi, Ndizi, Maharage, Viazi, Muhogo, Ulezi na ngano (Mazao ya chakula) na Kahawa, Pareto, Alizeti, Iliki na Soya (mazao ya biashara).

## 2.1. MALIASILI, RASILIMALI NA MAZINGIRA

Ileje ni moja ya sehemu zilizo na fursa nyingi za kiuchumi kutokana na upatikanaji wa maliasili upendezeshaji na kuvutia Wawekezaji ndani ya Wilaya. Kuwepo kwa Milima, viinuko na Mabonde kwa asili ya kijiografia, Mto Songwe, Luswisi, na Mito minge midogo yenyeuwezo wa kuchuruzisha maji yake kwa mwaka mzima pasipo kunyauka. Maporomoko ya maji katika kijiji cha Lusalala, Aridhi yenye rutuma na yenye uwezo wa kupanda mazao ya chakula na hata mazao ya kibiashara . Uoto wa asili, Misitu na Upandikizaji wa miti ni kivutio kikubwa katika uwekezaji na Ardhi iliyo jaa rutuba .

### JEDWALI NA.1 MAENEO KWA AJILI YA UWEKEZAJI WA VIWANDA

| Mgawanyo wa ardhi | | Eneo (Ha) | |
|---|---|---|---|
| 1 | Ardhi nayofaa kwa kilimo | 101,600 | |
| | Ardhi inayolimwa | **79,409** | |
| 2 | Ardhi iliyotengwa kwa uwekezaji | 1270 | |
| 3 | Ardhi yenye misitu ya hifadhi | 46,496.31 | |
| 4 | Eneo oevu | 3,415 | |
| 5 | Hifadhi za wanyama pori | 0 | |
| 6 | Makazi na matumizi mengine | 38,018.69 | |
| **Jumla** | | **190,800** | |
| **ARDHI YA UWEKEZAJI WA VIWANDA VIDOGO (SIDO)** | | | |
| Kiwanja na. 86 kitalu D Isongole | | Mita za mraba 3.345 | Kiwanda kidogo |
| Iwanja na. 87 kitalu D Isongole | | Mita za mraba 3.649 | Kiwanda kidogo |
| Iwanja na. 88 kitalu D Isongole | | Mita za mraba . 3.623 | Kiwanda kidogo |
| Iwanja na. 89 kitalu D Isongole | | Mita za mraba 3.202 | Kiwanda kidogo |
| **JUMLA NDOGO** | | **MITA ZA MRABA 13.817** | |

| MAENEO YA UWEKEZAJI WA VIWANDA VIKUBWA | | |
|---|---|---|
| Ipapa- Mjini Isongole | 23.664 | Uwekezaji wa kiwanda cha kusindika nafaka |
| MAENEO YA UWEKEZAJI WA VIWANDA VIKUBWA | | |
| Kijiji Cha Mapogolo | 8.054 | Kwa ajili ya umwagiliaji |
| Kijiji Cha Mbebe | 808.085 | Umwagiliaji |
| Kijiji Cha Ukumbilo | 63.335 | Umwagilaji |

*Chanzo Kitengo ya Ardhi*

## 3.0 USIMAMIZI WA UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI

Wilaya ina nia ya dhati ya kukuza uwekezaji wa ndani na nje ili kuchochea ukuaji wa uchumi, kupunguza umaskini na kupata faida ya kijamii na kiuchumi, hasa katika maeneo ya vijijini ambako watu wengi wanaishi. Kipengele hiki kinabainisha motisha mbalimbali za uwekezaji kulingana, na sera, taratibu za usimamizi na mfumo wa kisheria ili kuvutia wawekezaji na shughuli za kiuchumi.

### 3.1. Motisha ya Uwekezaji

Serikali ya Tanzania ya awamu ya tano inatambua umuhimu wa motisha ya kutosha na ufanisi katika kuvutia na kuongeza kiasi cha uwekezaji sahihi ndani na nje. malengo ya sera ya uwekezaji ni maalum katika kanuni za uwekezaji. motisha zinazotolewa ni kwa lengo la kuwa na ushindani na kuelekezwa Kwenye uwekezaji katika maeneo ambayo ni muhimu zaidi kwa maendeleo ya uchumi wa Tanzania na kukidhi mahitaji ya nchi.

Kwa kuzingatia sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi kiuchumi ya mwaka 2004, inaonesha dhamira ya dhati ya kukuza uchumi na kujenga mazingira ya uwekezaji kwa kutambua ya kwamba kiwango cha ukuaji wa Uchumi wa Tanzaniani kwa kutumia uwekezaji wa ndani ni kidogo na mazingira ya uwekezaji ambayo ndiyo chachu ya Uchumi endelevu, Hivyo basi niwazi Jitihada za kuwawezesha wananchi kushiriki kikamilifu katika shughuli za uchumi nchini ni muhimu ziendane na ukuaji wa uchumi unaojumuisha na kunufaisha Watanzania wengi, kuongeza vipato vyao pamoja na kuinua hali zao za maisha.

**Ili kukuza uchumi madhubuti na kujenga mazingira mazuri ya uwekezaji, mikakati ifuatayo itatekelezwa:-**

i. Kuzielekeza Sera za kisekta katika kuwawezesha wananchi kushiriki kikamilifu katika uchumi.
ii. Kuhakikisha kwamba hali ya amani na utulivu inadumishwa.
iii. Kuhakikisha kuwa Sera za kiuchumi zinakabiliana na mfumuko wa bei unadhibitiwa.

iv. Kuboresha miundombinu ili wananchi waweze kuitumia kwa gharama nafuu.
v. Kuwezesha kuingia ubia na kuboresha mitandao kati ya wananchi walio wengi na wawekezaji waliobobea ili kuhakikisha kwamba wananchi wananufaika na nguvu za wenye uwezo.

### 3.3. Ushirikiano na Sekta Binafsi na Umma

Ushirikiano wa Sekta Binafsi na Umma (PPP) ni chombo muhimu kwa serikali ya Tanzania cha kushawishi uwekezaji binafsi na kuboresha huduma za umma. Sera ya PPP ilitolewa mwaka 2009, Sheria ya PPP ilipitishwa mwaka 2010 na Kanuni zilipitishwa mwaka 2011.

Sheria mpya ya Ununuzi wa Umma (2011) inaweka sharti mahususi kwa ununuzi wa PPP kwa mapendekezo yaliyoombwa na yasiyoombwa.

### 3.4. Mazingira Wezeshi

Kwa sasa Halmashauri inashughulikia kuanzisha utaratibu mzuri wa miradi inayowezekana hasa katika sekta ya viwanda kwa kutafuta wawekezaji, ikiwa ni pamoja na kuandaa miongozo ya uendeshaji ya wa Miradi hiyo kati ya halmashauri na Mwekezaji, mkakati wa utekelezaji na mpango wa utekelezaji. Kwa urahisi na utekelezaji kwa wakati.

- **Ardhi**

Halmashauri Imetenga eneo kwa ajili ya Uwekezaji wa kiwanda kikubwa katika eneo la Ipapa mjini Isongole lenye ukubwa wa hekari 23,664.

**Miundombinu**

- **Barabara**
  Kuna barabara kuu ya kimataifa inayounganisha kati ya nchi jirani ya Malawi na Tanzania, inaweza kusafirisha malighafi pamoja na bidhaa kwa urahisi.
- **Umeme**
  Tayali maeno yaliyotengwa kwa ajili ya Uwekezaji wa Viwanda yamefikiwa na Umeme.
- **Maji**
  Huduma ya maji kwa ajili ya matumizi ya kiwanda inapatikana katika eneo hilo.
- **Mawasiliano**
  Mtandao wa Vodacom, Halotel, Tigo, TTCL na Airtel inapatikana vizuri kuwezesha mawasilano kwanjia ya intaneti na mawasilano kwa njia ya kawaida ya simu kwa maendeleo ya kiwanda hicho

## 3.5. UWEKEZAJI

### 3.5.1 UFUGAJI NYUKI NA KIWANDA CHA KUSINDIKA ASALI

Misitu ya Miombo ambayo iko katika wilaya ya Ileje, inafaa sana kwa ufugaji wa nyuki, hata hivyo pamoja na kuwa na misitu na nyuki wengi katika wilaya ya Ileje, ufugaji wa nyuki bado unafanywa kwa kiwango kidogo sana. Wilaya ya Ileje in nchi ya milima milima na hivyo shughuli itakayoweza kuinua kipato cha mwananchi wa kawaida ni ufugaji wa nyuki.



*Misitu ya Miombo inayofaa kwa ufugaji wa nyuki*

**Lengo:**

Kuwezesha na kuendeleza ufugaji nyuki na kuanzisha kiwanda cha kusindika asali.

**Ardhi kwa ajili ya mradi:**

Wilaya ya Ileje ina misitu ya asili yenye jumla ya Ha.46, 496.3, ambayo inafaa kwa ufugaji wa nyuki. Pia eneo la kilimo lenye Ha. 101,600, linafaa kwa ufugaji nyuki pamoja na kilimo (apiculture), Eneo la misitu lina uwezo wa kuweka mizinga 46,496,300 kwa wastani wa mizinga 1000 kwa Ha. Kila Mzinga una uwezo wa kuzalisha wastani wa lita 30 kwa mzinga kwa mwaka.

Mizinga 46,496, 300 x 30 = lita 1,394,889,000 kila lita inauzwa Ths.5000 kwa bei ya kijijini, mapato ya asali kwa mwaka ni Tshs.6, 974, 445,000,000.

Katika wilaya ya Ileje kuna vikundi 25 vinavyojishughulisha na ufugaji nyuki. Wilaya ina jumla ya mizinga ya nyuki ya kisasa 765 na mizinga ya kienyeji 12,482, inayoweza kuzalisha asali kiasi cha lita 765 x 30 = lita 22,950 x 5000 = Tshs.183, 600, 000 kwa mwaka. Kiwanda kikianzishwa kitahamasisha watu wengi kufuga nyuki na hivyo kuongza idadi ya wafugaji, idadi ya lita za asali na kuongeza kipato cha mwananchi wa kawaida.

**Mazingira ya Mradi :**

Misitu ya asili iliyopo wilayani Ileje inavutia na inafaa kwa ufugaji nyuki, pia hali ya kijiografia ya milima, hairuhusu mashamba makubwa, hivyo ufugaji wa nyuki ni mradi pekee wa kuinua kipato cha mkulima wa kawaida. Pia kuwepo kwa soko la ndani na nje ya nchi, ni kivutio kikubwa kwa wana Ileje kujikita katika ufugaji wa nyuki.

Mradi wa ufugaji nyuki ni rahisi kuanzisha na kuanza uzalishaji bada ya miezi sita. Bei ya kutengenza mzinga ni rahisi kwa wastani wa Tshs.40, 000 – 50,000 kulingana na mahali na aina ya mbao zitakazotumika. Mzinga ukishatundikwa unaweza kudumu kwa miaka 10 hadi 30 kutegemeana na matunzo. Ufugaji wa nyuki karibu na mashamba ya mazao kama vile mahindi, alzeti, maharage huongeza uchavushaji, na kuongeza mazao ya kilimo.

**Masoko:**

Soko la mazao ya nyuki hasa asali ni la kuridhisha ndani na nje ya nchi. Asali hutumika kama dawa, chakula na njia ya kujipatia kipato. Mazao ya nyuki kama vile nta, gundi ya nyuki, maziwa ya nyuki na sumu ya nyuki ni mazao yenye kuhitajika sana na yenye bei kubwa duniani.

### 3.5.2 USINDIKAJI MAJI YA KUNYWA

Mahitaji ya matumizi ya maji ya kunywa ya chupa yameendelea kuwa hitaji kubwa la watu wengi hapa Tanzania.

**Malengo na hoja**

**Lengo**


- Kuwepo kwa mahitaji ya maji ya kunywa ya chupa kwa watu zaidi ya wakazi 140,055 ambao niwakazi ndani ya wilaya na maeneo yote ya mkoa wa Songe na nchi ya Zambia na Malawa
- Kuboresha na kurasimisha rasilimali maji kwa kuongeza thamani.

**Mazingira ya Mradi**

Uwepo wa mito yenye maji ya kutosha mwaka mzima (kama vile mto Sange) ni kiashiria cha biashara zinazoweza kuwa na faida kutokana na kwamba chanzo cha maji ni moja ya marighafi mhimu katika uwekezaji wa maji ya kusindika.

Chanzo kinachopendekezwa kutumika katika usindikaji wa maji ni mto Sange unaopatikana kata ya Sange umbali wa km 74 kutoka makao makuu ya Wilaya (Itumba). Mto huu unakadiriwa kuwa na maji yenye uwingi wa mita za ujazo unaozidi 150 kwa saa wakati wa kiangazi na maji yake ni masafi hadi kufikia 25NTU (Turbidity) na yana ladha nzuri, hivyo utibuji wa maji kabla ya kusindikwa ni rahisi.

*Picha Na.1 Ikionyesha sehemu ya mto Sange*



### 3.5.3 KIWANDA CHA KUSINDIKA MAZIWA

Wilaya ina ng'ombe 38,789 wa asili, ng'ombe wa maziwa 809, mbuzi wa asili 31378, Mbuzi wa maziwa 284, kondoo5902, nguruwe 6368, Kuku wa kienyeji 153053 kuku wa mayai 2115, bata 567, sungura 736, njiwa 2,886, mbwa 3986, paka 1743, simbilisi 681 na punda 12. Wilaya hii ina jumla ya majosho 10 kati ya hayo sita tu ndio yanayofanya kazi. Pia, ina vituo vitatu vya mifugo ambapo kimoja ndicho kinachofanya kazi.

Jitihada za Halmashauri zimeendelea kufanyika kwa kuhakikisha kuwa sekta ya mifugo inaboreshwa ikiwa ni pamoja na kusamba ng'ombe wa maziwa, aidha Kwa kushirikiana na wadau wengine wa maendeleo imesaidia kuongeza uzalishaji wa ng'ombe wa maziwa.

#### Lengo

Ileje ina wastani wa wa ng'ombe wa kienyeji wapatao 38,789 na ng'ombe wa maziwa 809, inafanya jumla ya uzalishaji wa Maziwa lita 10,452.65 ambapo kiasi hicho hutumika kwa matumizi ya kawaida na kuandaliwa katika mfumo usio rasmi na hivyo kushusha thamani ya zao la maziwa.

#### Mazingira ya Mradi

Kukosekana kwa Mfumo rasmi wa Kuongeza thamani ya Zao la Maziwa ni fursa iliyowazi kwa ajili ya uwekezaji wa kiwanda cha kusindika maziwa. Maziwa yanayozalishwa ni mengi, hata hivyo hakuna kiwanda cha usindikaji wa maziwa hivyo maziwa mengi huaribika, na kuwapatia wafugaji hasara.

#### Lengo Mahsusi

- Kuwezesha Zao la maziwa kuongezeka thamani ndani ya wilaya.
- Kujenga soko la uhakika la zao la maziwa kwa wafugaji.
- Kurasimisha sekta ya Mifugo Kwa kuongeza usindikaji, ufungashaji kwa kutumia teknolojia za kisasa katika Mfumo wa Viwanda.

#### Masoko

Soko la maziwa ni la uhakika ndani na nje ya wilaya, kwani katika wilaya hakuna kiwanda cha kusindika maziwa, na hivyo msimu wa kipindi cha uzalishaji maziwa ni mengi na wakati wa uhaba wa maziwa, watumiaji wanakosa maziwa. Soko kubwa la maziwa liko Songwe, Mbeya na Dar es salaam.

### 3.5.4 KIWANDA CHA KUZALISHA VIFARANGA WA KUKU

Kuna takribani kuku 153, 053 wa kienyeji ndani ya wilaya. Ulaji wa kuku ni wastani wa kuku 500 kwa siku. Katika wilaya ya Ileje kuku wanaliwa pia katika mahoteli na katika migahawa.

**Lengo**

Lengo kubwa ni kuweka kiwanda cha kutotoleshea vifaranga vya kuku, ili kuweza kukidhi mahitaji ya soko la ndani na nje ya wilaya. Vifaranga wanahitajika sana katika maeneo mengi ya nchi yetu kama vile tunduma, mbozi, Iringa, Morogora na Dar Es Salaam.

**Mazingira ya mradi**

Ileje ni maarufu kwa kuzalishaji wa kuku wa kienyeji wanaojulikana kwa jina mkorongo (Black australop). Kuku hawa wamekuwa na soko kulingana na sifa ya kuvumilia magojwa, Rangi yake nyeusi ya kuvutia, Umbo lake kubwa, hivyo kuwa na nyama nyingi, wanaweza kufugwa kwa njia ya kisasa na kienyeji, pia wana uwezo mkubwa wa kutaga mayai na vifaranga wake hukua haraka.

**Masoko**

Masoko ya vifaranga vya kuku yapo wazi, ndani na nje ya wilaya ya Ileje. Hii ni kwa sababu ulaji wa kuku na mayai unakua na kuongezeka kila siku. Kiwanda cha kutotolesha vifaranga kitakuwa chachu ya wananchi wa Ileje, kuongeza ufugaji wa kuku na hivyo kuongeza kipato cha mwananchi wa kawaida na pato laTaifa kwa ujumla.

### 3.5.5 KIWANDA CHA KUSINDIKA ALIZETI (DOUBLE REFINING PROCESSING PLANT)

Wilaya ya Ileje inazalisha mazao mbalimbali yakiwemo ya chakula na biashara, mazao ya chakula ni pamoja na mahindi, maharage, ulezi, viazi mvirngo, karanga, soya,viazi vitamu na mpunga, ambapo mazao ya biashara ni alizeti, kahawa, pareto, Iliki na kiasi kidogo cha zao la kokoa

**Mazingira ya Mradi**

Ileje ina eneo la Ha 16,640 linalofaa kwa kilimo cha zao la alizeti, uzalishaji wa zao la alizeti kwa sasa siyo mkubwa, hata hivyo jitihada ya Halmashauri ni kuhakikisha wananchi wanaongeza uzalishaji wenye tija na maeneo yanapanuliwa kwa ajili ya kilimo cha zao hili kama zao hili limeonyesha kuongeza kipato kwa wananchi, kupata mafuta kama lishe na mazao yanayotokana na alizeti kama vile mashudu kwa ajili ya chakula cha mifugo. Eneo kwa ajili ya kujenga kiwanda/ viwanda limetengwa na kupimwa katika mji mdogo wa Isongole ambalo linamilikiwa na shirika la viwanda vidogo (SIDO).

Kwa sasa kuna jumla ya viwanda vidogo 11 vya kukamua alizeti vinavyomilikiwa na watu binafsi na taasisi za madhehebu ya dini katika vijiji vya Mbebe, Ikumbilo, Msia, Isongole na Itumba.

### Lengo
Lengo la mradi huu ni kuongeza upatikanaji wa mafuta ya alizeti yaliyochujwa vizuri na kuongezewa thamani hadi kukidhi viwango vya soko la ndani na nje ya nchi. Kuwepo kwa kiwanda chenye kuchuja mafuta vizuri kutachochea uzalishaji wa zao la alizeti na hivyo kuongeza upatikanaji wa mazao ya ziada kama vile mashudu kwa ajili ya chakula cha mifugo.

### Masoko
Kufuatia umuhimu wa zao hili na mazao yanayotokana na alizeti, kuna hitaji kubwa la bidhaa zinazozalishwa hivyo kuanzishwa kwa kiwanda cha kusindika alizeti itasaidia katika kuongeza thamani ya bidhaa hii na kuwezesha ajira katika mnyororo mzima wa uzalishaji wa zao la alizeti, takribani kiwanda kinaweza kuwapatia ajira zaidi ya watu 100. Kwa sasa soko lipo ndani ya Wilaya na kiasi kingine pamoja na mashudu huuzwa katika Wilaya tunazopakana ikiwemo, Tunduma, Momba na Mbozi, na baada ya kuazishwa kwa kiwanda cha kukamua vizuri alizeti (double refinery plant), soko litakuwa ndani na nje ya nchi.

### 3.5.6 KIWANDA CHA KUSINDIKA UNGA (MEDIUM FLOUR PROCESSING PLANT)
Zao la mahindi ni miongoni mwa mazao ya chakula katika wilaya ya Ileje kama zao kuu la chakula, aidha zao hili hutumika kama zao la biashara kwa kuuza ziada inayozalishwa.

### Mazingira ya mradi
Eneo linalolimwa zao la mahindi kwa mwaka ni wastani wa Ha 24,362, ambapo eneo linalofaa kwa kilimo ni Ha 101,600, na eneo linalolimwa kwa sasa kwa mazao yote ni Ha 79,409, ambapo uzalishaji kwa mwaka hufikia zaidi ya tani 90,000.
Mahitaji ya chakula kwa wananchi wa Ileje ni tani 42,017 kwa mwaka hivyo kuwa na ziada ya mahindi kwa kila mwaka kwa kiasi cha zaidi tani 48,000.

### Masoko
Masoko yatakuwa ndani na nje ya wilaya, pamoja na nchi tunazopakana nazo, kama vile Malawi na Zambia, pamoja na mkoa inayopata mvua kidogo katika nchi yetu.
Kiwanda cha kusindika unga kitasaidia kuongeza mnyororo wa thamani katika zao la mahindi na kuchochea uzalishaji wa zao hili na hivyo kuinua kipato na kuwezesha ajira kwa makundi ya vijana.



*Picha ikionyesha ununuzi wa zao la mahindi katika soko la Isongole wilaya ya Ileje.*

### 3.5.7 KIWANDA CHA KUZALISHA MAKAA YA MAWE

#### MAKAA YA MAWE

Makaa ya mawe yanapatikana kwa wingi katika eneo la kiwira ambalo kijiografia lipo katika wilaya ya Ileje.

#### Mazingira ya mradi.

Uchimbaji wa makaa ya mawe katika eneo la Ileje ulianza kufanyika mwaka 1984, kazi hii ikisimamiwa kwa ushirikiano kati ya serikali ya Tanzania na Serikali ya China.
Ilipofika mwaka 1990, uchimbaji na uzalishaji wa makaa ya mawe pamoja na uzalishaji wa umeme kiasi cha MW.6 ulikoma. Eneo hili la makaa ya mawe yaani Mlima kabulo ni la Misitu ya Hifadhi ya Tanzania Forest Service na limehifadhiwa kisheria.

Mpaka sasa mradi huu umesima. Hata hivyo eneo liliokuwa linachimbwa madini haya ni dogo sana ukilinganisha na rasilimali iliyoko ya makaa ya mawe. Eneo lililokuwa linachimbwa makaa ya mawe lipo katika mlima Ivogho, lakini hazina ya makaa ya mawe imeendelea mpaka katika mlima Kabulo ambapo kuna takribani ha.7,250. Tafiti zinaonyesha kuwa makaa ya mawe yaliyopo Kiwira yanafaa zaidi kwa ajili ya uzalishaji wa umeme kuliko kutumika katika viwanda vya kuzalishia saruji, chai nk.

#### Lengo la mradi.

Lengo la mradi huu ni kuzalisha umeme kwa kutumia makaa ya mawe. Mradi huu utakuwa na kazi kuu mbili ya kwanza ni kuchimba na kuandaa makaa ya mawe na kazi ya pili ni kuzalisha umeme kwa kutumia makaa ya mawe.

#### Masoko

Masoko kwa ajili ya bidhaa hii ambayo ni nishati ya umeme itauzwa TANESCO na kuingizwa katika grid ya Taifa, na baadhi ya nishati kidogo itatumika kuendesha kiwanda cha makaa ya mawe.

## 4.0 HITIMISHO

Ili kuboresha na kufanikisha uwekezaji wa viwanda Halmashauri imeweka mipango mizuri ya kuratibu utaratibu wa uanzishwaji wa viwanda ikiwa ni pamoja na kusimamia na kutekeleza sera ya Mazingira ya mwaka 1998, sera ya uwezeshaji wananchi kiuchumi ya mwaka 2004, sera ya kilimo na masoko ya mwaka 2008, sera ya taifa ya uwekezaji na Dira ya Maendeleo ya taifa. Hata hivyo usimamizi wa sheria na mipango mikakati ya halmashauri, pamoja na utekelezaji wake Vitakuwa ni kichocheo kikubwa cha ukuaji wa kiuchumi, kuongeza ajira kwa vijana na wanawake ili kuongeza ushindani wa kiuchumi ndani na nje ya wilaya.

Ni wajibu wetu Viongozi na wataalamu mbalimbali wa kila sekta kuanzia ngazi ya mitaa/vijiji hadi Mkoa na taifa, kushawishi na kuhamasisha watanzania kuwekeza katika sekta ya viwanda, biashara na ushirika ili kuongeza kasi zaidi ya ukuaji wa kiuchumi kwa mwananchi mmoja mmoja.

***Ileje ya viwanda inawezekana, kila mmoja atimize wajibu wake***

Naomba kuwasilisha,

HAJI M.MNASI
Mkurugenzi Mtendaji(W),
**ILEJE**